

**Jibu:** Tureje..

*Luka 7:37 “Na tazama, mwanamke mmoja wa mji ule, aliyekuwa mwenye dhambi, alipopata habari ya kuwa ameketi chakulani katika nyumba ya yule Farisayo, alileta chupa ya MARIMARI yenye marhamu”.*

“**Marimari**” ni jina lingine la “**Marumaru**”, kwahiyo popote katika biblia palipotajwa Marimari ni sawasawa na Marumaru. Na marimari ni mawe ya kaboni, ambayo yanatumika katika urembo wa ujenzi, mawe haya ni maarufu sana kwa kutengenezea Tiles za ukutani au chini.

Vile vile yanatumika kutengenezea baadhi ya vyombo vya kinakshi mfano wa cha hicho cha mwanamke katika *Luka 7:37* n.k

Maandiko mengine yanayotaja Marimari ni pamoja na **1Nyakati 29:2, Wimbo ulio bora 5:15 na Ufunuo 18:12...** lakini andiko lililotaja Marimari kama Marumaru ni **Esta 1:6.**

Je umempokea **BWANA YESU**, na kubatizwa katika ubatizo sahihi?.. Je unatambua kuwa tunaishi katika majira ya kurudi kwa YESU mara ya

pili, na wakati wowote parapanda ya mwisho inalia?

Je macho yako yanaona hayo yote?.. kama huyaoni hayo basi fahamu kuwa upo gizani na yule mkuu wa giza (*shetani*) amekupofusha macho ili usione, Leo harakisha kupokea msaada kutoka kwa **YESU**.

Ikiwa utahitaji kumpokea YESU leo, basi fuatiliza sala hii hapa

>>**KUONGOZWA SALA YA TOBA**

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

**<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>**

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

**Mafundisho mengine:**

**Sala ya baraka (Hesabu 6:24-26).**

**NINI MAANA YA KUWA MKRISTO?**

**Ni lazima mtu aongozwe sala ya toba ili awe ameokoka?**

**SI KILA KILICHO HALALI KINAFAA.**

**TOBA IGUSAYO MOYO WA BWANA.**

**Rudi Nyumbani**

Share on:

WhatsApp

[Print this post](#)